TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578

KANUNI ZA LIGI NA USAJILI

LIGI ZOTE

ZINAZOCHEZWA NA KUSIMAMIWA

AU KURUHUSIWA NA TAVA

NOVEMBA 2023

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578

YALIYOMO

YALIYOMO.....2
Utangulizi.....3
Msimu wa mashindano.....3
Msimu wa mapumziko.....3
msimu wa mapumziko mwaka huu 2022.....3
Msimu wa mashindano awamu ya kwanza.....3
Msimu wa mashindano kwa mwaka 2023.....4
Dirisha dogo la usajili.....4
Msimu wa mashindano awamu ya pili.....4
Muhimu.....4
Mfumo wa usajili.....4
Usajili wa msimu kwaajili ya takwimu za msimu (usajili mkuu).....4
Usajili wa timu (Volleyball & Beach Volleyball).....5
Mahitaji ya usajili.....5
Usajili wa wachezaji (Volleyball & Beach Volleyball).....5
Mahitaji ya usajili.....6
Usajili wa makocha (Volleyball & Beach Volleyball).....6
Mahitaji ya usajili.....6
Usajili wa waamuzi (Volleyball & Beach Volleyball).....6
Mahitaji ya usajili.....7
Usajili wa taasisi binafsi (Foundation/ Academy).....7
Mahitaji ya usajili.....7
Usajili wa vituo/ shule za kukuza vipaji.....7
Mahitaji ya usajili.....7
Muhimu.....8
Ada za usajili wa msimu (Usajili muu/ seasonal registration).....8
Kanuni muhimu za kuzingatia kukamilisha usajili.....8
Mgawanyo wa ada za usajili.....9
Usajili wa muda (Temporary transfer).....9
Dirisha dogo la usajili.....9
Kanuni za dirisha dogo la usajili.....9
Usajili wa michuano ya wazi (Open tournaments).....10
Kanuni za usajili wa michuano ya wazi.....10
Timu za kitaasisi.....10
Vilabu vya ndani ya nchi.....10
Vilabu vya nje ya nchi.....10
Masharti muhimu.....11
Ada za usajili wa muda (Temporary transfer fee).....11
Usajili wa mchezaji kutoka nje ya nchi kwaajili ya ligi.....11
Muhimu.....12
Utaratibu wa malipo.....12
Haki na usimamizi wa hadhi za wachezaji.....12
Hitimisho.....14
Namna ya kuingia kujisajili(kutumia kompyuta).....15
Fomu ya makubaliano kati ya mchezaji na timu.....21

UTANGULIZI

Chama cha mpira wa wavu Tanzania kinaendelea kuboresha Sheria, Kanuni na Miongozo itakayo ongoza shughuli zote za mpira wa wavu nchini, ikiwa ni pamoja na kuhuisha na kuimarisha uwajibikaji wa kila mdau anayejishirikisha na mpira wa wavu. Ifahamike kwamba mpira wa wavu unapata ushirikishwaji kuanzia kwa mchezaji mwenyewe, viongozi wa timu, uongozi wa chama cha wilaya, uongozi wa chama cha mkoa, uongozi wa serikali, washabiki wa mchezo wa wavu, waandishi wa habari na wadhamini kwa namna mbalimbali.

Sheria, Kanuni na Miongozo itakuwa na madhumuni ya kusimamia haki na wajibu wa kila mshiriki huku ikilinda hadhi zao nyakati zote. Kwa nyakati zote, utekelezaji na usimamizi wa Sheria, Kanuni na Miongozo utaanzia ngazi ya Timu/ Klabu, Wilaya, Mkoa, Kamisheni husika ambapo ngazi ya Mwisho ni ofisi ya Sekretarieti ya TAVA.

1. **MSIMU WA MASHINDANO**
   Chama cha mpira wa wavu Tanzania – TAVA kimeweka kalenda ya kuanza na kumalizika kwa msimu wa mashindano, kwanamna yoyote msimu wa mwaka utakuwa umegawanyika katika makundi yafuatayo;

1.1 Msimu wa mapumziko (off season)

Msimu wa mapumziko utaanza pale ligi inapomalizika, kwa mujibu wa kalenda kipindi hiki kitakuwa kati ya mwezi wa nane (8) na mwezi wa kumi (10). Matukio yatakayohusika katika kipindi hiki cha mapumziko ni ***usajili*** na maandalizi kwaajili ya msimu unaotarajiwa kuanza.

1.1.1 Msimu wa mapumziko mwaka huu wa 2023

Kwasababu za kimfumo, Msimu wa mapumziko mwaka huu wa 2023 umeanza baada ya ligi ya taifa kuisha (30/09/2023) na utamalizika Disemba 31, 2023. Wakati wa mapumziko kutahusisha usajili utakaoanza Novemba 13, 2023 na kudumu kwa siku 30 tangu tarehe ya dirisha kufunguliwa.

1.2 Msimu wa mashindano awamu ya kwanza

Msimu wa mashindano utafunguliwa tarehe 14 mwezi wa kumi (14 Octoba), na fainali za shindano la Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere zitakuwa maalum kufunga msimu uliopita. Awamu hii ya kwanza itakuwa ikimalizika mwezi wa tatu tarehe 31 (31 Machi) ilikuruhusu mapumziko mafupi yatakayo ambatana na usajili mdogo kwa wachezaji. Ligi zote zitakazokuwa zinaendelea mikoani zitapaswa kuzingatia kanuni hizi ili kuruhusu uratibu wa mfumo wa usajili kitaifa, ikiwa ni pamoja na uhamisho wa wachezaji.

1.2.1 **Msimu wa mashindano kwa mwaka 2024**

Tofauti na kanuni hapo juu, kutokana na uboreshaji wa mifumo ya TAVA; msimu wa mashindano utaanza mwezi Januari (tarehe itatangazwa baada ya usajili kukamilika) na kumalizika mwezi Mei, 2024. Kumalizika huku kutahusisha mashindano yote ya mikoa pamoja na fainali/ play off zake ngazi ya mkoa au kanda kadiri itakavyoratibiwa na maeneo husika.

1.3 Dirisha dogo la usajili

Dirisha dogo la usajili litafunguliwa tarehe moja mwezi wa nne (01 Aprili) na kuwa wazi kwa wiki mbili hadi tarehe kumi na nne mwezi wa nne (14 Aprili).

1.4 Msimu wa mashindano awamu ya pili

Msimu wa mashindano awamu ya pili utafunguliwa tarehe 19 mwezi wa nne, na shindano la kwanza litakuwa ni la Muungano. Pamoja na michuano hiyo, awamu hii ya pili itamalizika mwezi wa tano tarehe 30 (30 Mei) ikiwa ni kumalizika kwa ligi na msimu (Rejea kifungu 1.2.1).

MUHIMU

*Kalenda hii ya kuanza na kumalizika kwa msimu Pamoja na matukio ya ndani yake tarehe zinaweza kubadilika kulingana na hali na mahitaji yatakavyokuwa kwa wakati huo au sababu zisizozuilika. Taarifa maalumu ya kubadilika kwa tarehe zitatolewa na **Katibu Mkuu** kwa utaratibu maalum.*

2. MFUMO WA USAJILI

Waraka huu ni kwa minajili ya kuweka muongozo wa kusimamia usajili wa Mchezaji mmoja mmoja, Klabu, Makocha na Waamuzi. Katika usimamizi wa michezo nchini na dunia nzima; usajili wa mchezaji na timu ni utaratibu muhimu ambao huleta hadhi ya timu husika, mchezaji mmoja mmoja au wachezaji kwa ujumla, Waamuzi na Makocha wanaofundisha vilabu/ taasisi mbalimbali. Muongozo wa usajili pia utahusika wakati wa michakato ya uhamisho wa wachezaji kati ya timu na timu ambapo unatazamiwa kulinda hadhi na kuleta chachu ya kuinua na kukuza vipaji nchini. Usajili utahusu Timu/ Vilabu, Taasisi zinazojihusisha na mpira wa wavu (foundation), vituo vya ukuzaji na uendelezaji wa watoto (shule), Wachezaji, Makocha, na Waamuzi.

Muongozo huu wa usajili utatumika kuzingatia kalenda ya msimu wa mashindano wa mwaka husika, utahusu makundi mawili;

2.1 <u>Usajili wa Msimu kwa Ajili ya Takwimu za Msimu (Usajili Mkuu)</u>

Usajili wa msimu kwaajili ya takwimu za msimu (usajili mkuu) utahusika kusajili washiriki wafuatao;

2.1.1 **Usajili wa timu (Volleyball & Beach volleyball),**

Kila klabu inayojihusisha na mpira wa wavu nchini ni lazima ijisajili katika mfumo wa kielectroniki wa TAVA, vilabu hivyo vinaweza vikawa ni vilabu binafsi, vilabu vinavyobeba majina ya taasisi za serikali au binafsi (vyuo, mashirika na vikosi), na vituo maalumu vya malezi. Kwaminajili ya kuweka kumbukumbu sawa, klabu iliyo katika kundi lolote katika mabano, itapaswa kuambatanisha nyaraka inayoonesha uanzishwaji wake (Katiba ya klabu).

Klabu iliyosajiliwa na kuwasilisha nyaraka zote za usajili toka mamlaka za serikali, TAVA itatoa namba ya usajili ya kitaifa na itaisajili katika mfumo wa tarifa wa FIVB (VIS) na kupatiwa namba ya usajili toka shirikisho la mpira wa wavu duniani (FIVB namba) kwaajili ya kutambulika kimataifa.

Mahitaji ya usajili;

i. Barua kwenda kwa Mwenyekiti wa Mkoa kuomba kusajiliwa, ipitishwe (kusainiwa na kugongwa muhuri) na Mwenyekiti wa Wilaya husika, (kwa Vyama vya wilaya vilivyo hai)
ii. Andiko linaloonesha orodha ya viongozi wa klabu (Meneja, Katibu, Mhazini, Wajumbe wasiopungua 3), viongozi wote wasaini na kuweka namba zao za simu,
iii. Risiti ya benki kuonesha malipo ya ada ya usajili wa msimu kwa TAVA,

2.1.2 **Usajili wa Wachezaji (Volleyball & Beach volleyball),**

Kila klabu itakayokuwa imejisajili kushiriki katika mashindano yanayosimamiwa na TAVA kwa ngazi zote itapaswa kufanya usajili wa wachezaji inaokusudia kuwatumia katika msimu husika, fomu maalum zitajazwa kupitia mfumo wa kielektroniki wa TAVA ambapo mchezaji atapatiwa leseni itakayokuwa inafuatiliwa wakati wote wa msimu.

(Wachezaji watakaosajiliwa hawatahusika kwenye shindano la kumbukumbu ya Mwl. Nyerere. Wachezaji watakuwa huru na kusimamiwa na kanuni za shindano hilo)

Mchezaji aliyesajiliwa na TAVA na kuambatanisha nyaraka zote zinazostahili na kupatiwa leseni ya kitaifa, TAVA itamsajili katika mfumo wa kimataifa (VIS) ambapo atapatiwa namba ya usajili toka shirikisho la mpira wa wavu duniani (FIVB namba) kwaajili ya kutambulika kimataifa, namba hiyo itahusika katika maisha yake yote ya uchezaji wa mpira wa wavu.

Mahitaji ya usajili;

i. Mkataba/ makubaliano baina ya klabu na mchezaji, mkataba unapaswa uoneshe muda wa kuanza na kuisha kwa makubaliano, Maslahi, haki na wajibu wa kila upande,
ii. Ikiwa mchezaji siyo raia wa Tanzania, ziambatanishwe nyaraka zinazo mruhusu kuingia nchini ikiwa ni pamoja na kibali cha kazi toka mamlaka zinazohusika nchini, au nyaraka zinazohalalisha uwepo wake nchini,
iii. Kwa wachezaji wenye umri zaidi ya miaka 18, picha aina ya paspoti saizi ya mchezaji, namba ya NIDA/ Leseni ya udereva/ kitambulisho chochote kinachotambulika na mamlaka za kitaifa,
iv. Kwa wachezaji wenye umri chini ya miaka 18, cheti cha kuzaliwa pamoja na barua ya ridhaa ya mzazi/ mlezi wa mtoto au shule anayosoma mtoto,
v. Risiti ya benki kuonesha malipo ya ada ya usajili wa msimu kwa TAVA,

2.1.3 **Usajili wa Makocha (Volleyball & Beach volleyball),**

Yeyote aliyepata mafunzo ya ukocha atapaswa kujisajili katika mfumo wa kielektroniki wa TAVA ambapo kocha ataambatanisha vyeti vyake vya mafunzo. Pamoja na taarifa hizi, TAVA itampatia leseni kwaajili ya kumruhusu kufanya shughuli za ukocha baada ya kukidhi vigezo vya usajili.

Kocha aliyesajiliwa na TAVA na kuambatanisha nyaraka zote zinazostahili na kupatiwa leseni ya kitaifa, TAVA itamsajili katika mfumo wa kimataifa (VIS) ambapo atapatiwa namba ya usajili toka shirikisho la mpira wa wavu duniani (FIVB namba) kwaajili ya kutambulika kimataifa, namba hiyo itahusika katika maisha yake yote ya ukocha wa mpira wa wavu.

Mahitaji ya usajili;

i. Cheti cha kufuzu mafunzo ya taaluma ya Ukocha,
ii. Picha aina ya pasipoti saizi, namba ya NIDA/ Leseni ya udereva/ kitambulisho kinachotambuliwa na mamlaka za kitaifa,
iii. Risiti ya benki kuonesha malipo ya ada ya usajili wa msimu kwa TAVA,

2.1.4 **Usajili wa Waamuzi (Volleyball & Beach volleyball).**

Yeyote aliyepata mafunzo ya uamuzi atapaswa kujisajili katika mfumo wa kielectroniki wa TAVA ambapo muamuzi ataambatanisha vyeti vyake vya mafunzo. Pamoja na taarifa hizi, TAVA itampatia leseni kwaajili ya kumruhusu kufanya shughuli za uamuzi baada ya kukidhi vigezo vya usajili.

Muamuzi aliyesajiliwa na TAVA na kuambatanisha nyaraka zote zinazostahili na kupatiwa leseni ya kitaifa, TAVA itamsajili katika mfumo wa kimataifa (VIS) ambapo atapatiwa namba ya usajili toka shirikisho la mpira wa wavu duniani (FIVB namba) kwaajili ya kutambulika kimataifa, namba hiyo itahusika katika maisha yake yote ya uamuzi wa mpira wa wavu.

Mahitaji usajili;

i. Cheti cha kufuzu mafunzo ya taaluma Uamuzi,
ii. Picha aina ya pasipoti saizi, namba ya NIDA/ Leseni ya udereva/ kitambulisho kinachotambuliwa na mamlaka za kitaifa,
iii. Risiti ya benki kuonesha malipo ya ada ya usajili wa msimu kwa TAVA**,**

2.1.5 Usajili wa taasisi binafsi (Foundation/ Academy)

Academy na Foundation zitakazosajiliwa katika kipengele hiki ni zile zilizofunguliwa na wadau zenye mlengo wa kujishughulisha na mchezo wa wavu, ambazo zinapaswa kusajiliwa na wizara ya Afya au BMT kwa mujibu wa sheria. Hii haihusiani na vituo vya mafunzo ya watoto vilivyopo kwenye shule kadhaa nchini.

Mahitaji ya usajili;

i. Barua ya utambuzi toka kwa Mwenyekiti wa Mkoa kupitia Wilaya husika,
ii. Cheti cha usajili toka BMT au wizara ya Afya,
iii. Katiba inayoonesha muundo wa uongozi, akaunti na mipaka ya utendaji/ majukumu yake,
iv. Andiko linaloonesha orodha ya viongozi, wawe wamesaini na kuweka namba za simu wanazopatikana. Andiko lioneshe muhuri wa ofisi

2.1.6 Usajili wa vituo/ shule za kukuza vipaji

TAVA imeandaa mfumo rasmi utakao vitambua vituo/ shule zinazolea watoto kwaajili ya kuandaa wachezaji. Mfumo huu utakitambua kituo/ shule na Wakati huohuo ukimsajili mtoto kwaajili ya kufuatilia makuzi yake kwafaida yake na taifa kwaujumla.

Mahitaji ya usajili;

i. Barua ya utambuzi toka kwa Mwenyekiti wa Mkoa kupitia Wilaya husika,
ii. Barua ya utambuzi toka kwa Afisa Elimu wa Halmashauri husika,
iii. Orodha ya watoto waliosajiliwa katika kituo hicho ioneshe majina, umri, na jinsia

MUHIMU:

Aina yoyote ya usajili utafanyika kupitia fomu maalum za kielektroniki zitakazotumwa kwa vyama vya mikoa, ambapo uongozi wa mkoa utawajibika kuzituma kwa viongozi wa vilabu vilivyopo mkoani kwake ambao wataingiza taarifa za Wachezaji, Waamuzi, Makocha na Vilabu kwenye mfumo huo wa kielektroniki wa chama cha mpira wa wavu Tanzania – TAVA. Wote watakaosajiliwa katika timu husika watapatiwa leseni toka TAVA na namba toka shirikisho la mpira wa wavu duniani (FIVB Namba) nakutambulika kama wachezaji halali kwa ajili ya kushiriki shughuli za mchezo wa wavu kwa msimu wa mashindano wa mwaka 2023/ 24.

2.1.7 **Ada za Usajili wa Msimu (Usajili Mkuu/ seasonal registration);**

2.1.7.1 Usajili wa mchezaji (Mtanzania) kwa mwaka ni	Tsh. 5,000/=
2.1.7.2 Usajili wa mchezaji (Wakigeni) kwa mwaka ni	Tsh. 50,000/=
2.1.7.3 Usajili wa klabu kwa mwaka ni	Tsh. 30,000/=
2.1.7.4 Usajili wa kocha Daraja III kwa mwaka ni	Tsh. 30,000/=
2.1.7.5 Usajili wa kocha Daraja II na I kwa mwaka ni	Tsh. 20,000/=
2.1.7.6 Usajili wa muamuzi wa Daraja A kwa mwaka ni	Tsh. 20,000/=
2.1.7.7 Usajili wa muamuzi wa kitaifa kwa mwaka ni	Tsh. 10,000/=
2.1.7.8 Usajili wa muamuzi mwanafunzi wa kimataifa kwa mwaka ni	Tsh. 10,000/=

2.1.8 **Kanuni Muhimu za kuzingatia kukamilisha usajili**

2.1.8.1 Kila timu itakuwa na haki ya kusajili wachezaji wa msimu wasiopungua kumi na nne (14) na wasiozidi ishirini (20),

2.1.8.2 Timu itakuwa na haki ya kusajili wachezaji wakigeni wasiozidi watano (5), Wachezaji hawa watakuwa ndani ya idadi ya wachezaji ishirini (20),

2.1.8.3 Katika wachezaji watano wakigeni, ni wachezaji wasiozidi watatu pekee wataruhusiwa kucheza/ kuwa uwanjani kwa pamoja katika mechi inayoendelea,

2.1.8.4 Kutakuwepo na makubaliano kati ya timu atokapo mchezaji na timu aendako, aidha timu au mchezaji hatoruhusiwa kuanza mazungumzo ya uhamisho kabla dirisha la usajili halijafunguliwa na TAVA, bila kuathiri dirisha la usajili, mazungumzo ya usajili kwa mchezaji asiye na mkataba/ makubaliano na timu yoyote yanaweza kufanyika wakati wowote,

2.1.8.5 Ada ya uhamisho au usajili ilipwe kabla ya mchezaji kuanza kuitumikia timu yake, na

2.1.8.6 Mchezaji anayesajiliwa atapewa leseni baada ya kukamilisha taratibu zote za usajili au uhamisho. Kwasababu za kulinda hadhi za wachezaji, mchezaji hataruhusiwa kuitumikia klabu nyingine bila TAVA kujua, na kwa vyovyote vile utaratibu utafuata usajili wa muda kama inavyoelezwa katika waraka huu kanuni ya 2.2 (Usajili wa Muda).

2.1.9 **Mgawanyo wa Ada za Usajili (Registration Fee)**

Ada za usajili (registration fee) zitagawanywa kwa ngazi zote zinazohusika katika kusimamia mchezo wa wavu. Mgawanyo huo utakuwa kamaifuatavyo;

2.1.9.1 Chama cha Mkoa kilichosajiliwa kitapata asilimia arobaini (40%)

2.1.9.2 Chama cha taifa kitapata asilimia sitini (60%)

2.1.9.3 Klabu anayotoka na anayokwenda watafanya makubaliano ya gharama za uhamisho wa mchezaji na kulipana wenyewe.

MUHIMU:

2.1.9.4 Makubaliano yoyote kati ya hayo hapo juu lazima yafanyike kwa maandishi na kuwasilisha nakala ya mkataba/ makubaliano ya uhamisho kwenye chama cha mpira wa wavu taifa – TAVA kupitia chama cha mkoa husika.

2.1.9.5 Malipo yote kwa asilimia miamoja (100%) yalipwe kupitia akaunti ya TAVA na gawio la asilimia arobaini (40%) toka TAVA kwenda chama cha mkoa yatafanyika kupitia akaunti ya mkoa husika, ikiwa chama hakina akaunti, gawio lake litabaki TAVA hadi hapo itakapofunguliwa akaunti ya mkoa husika kupitia viongozi wake.

2.1.9.6 Gawio la chama cha mkoa litafanyika ndani ya mwaka/ msimu husika wa usajili. Chama kisipowasilisha maombi ya malipo yanayoambatana na akaunti ya malipo ndani ya msimu huo, malipo hayo yatakuwa yamefutika moja kwa moja (forfeited). Malipo ya gawio hayatavuka mwaka/ msimu wa usajili uliofanyika.

2.2 <u>Usajili wa Muda (Temporary Transfer)</u>

Usajili wa muda umegawanyika katika katika makundi mawili;

2.2.1 **Dirisha dogo la usajili**

Dirisha dogo la usajili litafunguliwa tarehe 01 Aprili na kufungwa tarehe 14 Aprili.

Kanuni za dirisha dogo la usajili

2.2.1.1 Kila timu itakuwa na haki ya kusajili na kupunguza wachezaji wasiozidi wawili (2), Aidha pamoja na usajili huu wa muda, idadi ya wachezaji itabaki kuwa ileile wasiopungua kumi na nne (14) na wasiozidi ishirini (20),

2.2.1.2 Kutakuwepo na makubaliano kati ya timu atokapo mchezaji na timu aendako, aidha timu au mchezaji hatoruhusiwa kuanza mazungumzo ya uhamisho kabla dirisha dogo halijafunguliwa na TAVA, na

2.2.1.3 Ada ya uhamisho ilipwe kabla ya mchezaji kuitumikia timu yake mpya.

2.2.2 **Usajili wa michuano ya wazi (Open tournaments)**

Michuano ya wazi (Open tournaments) ni michuano inayoendeshwa kufuatia tukio maalumu, au michuano inayoandaliwa na taasisi washirika wa TAVA nchini. Pamoja na kuwa michuano hii ni ya wazi, bado adhma ya TAVA kusimamia kanuni na taratibu inabakia palepale. Vilabu vinavyojiandaa kushiriki michuano kama hii ni lazima vikidhi vigezo vya kisheria na kupata uhalali wa kushiriki, vigezo hivyo vitakuwa vimeainishwa kwenye barua ya mwaliko.

Kanuni za Usajili wa michuano ya wazi

2.2.2.1 Klabu inayotarajia kushiriki michuano ya wazi itakuwa na nafasi ya kusajili Wachezaji ishirini (20) kama kanuni ya usajili wa kudumu unavyojieleza,

2.2.2.2 Hakutakuwa na ada ya usajili wa mchezaji yeyote, isipokuwa malipo ya ushiriki wa klabu katika mashindano yaliyo andaliwa,

2.2.2.3 Taarifa za wachezaji wakigeni ziwasilishwe TAVA kwa maandishi kabla ya mchezaji kushiriki mashindano, taarifa hizo ni pamoja na Paspoti ya mchezaji,

2.2.2.4 Malipo ya ushiriki wa klabu katika mashindano ya wazi (Open tournament) yatakuwa yameainishwa katika barua za mialiko wa mashindano husika, Kwasababu za makusudi, TAVA inaainisha sifa zitakazo iweka klabu shiriki katika kundi litakalostahili kwaajili ya kufanya malipo kama ifuatavyo;

2.2.2.4.1 ***Timu za kitaasisi***

Hizi ni timu zinazotoka katika taasisi au mashirika ya kiserikali ndani ya nchi ya Tanzania. Mfano Jeshi, vyuo na mashirika.

2.2.2.4.2 ***Vilabu vya ndani ya nchi***

Hivi ni vilabu vyote visivyohusiana na orodha tajwa hapo juu (Taasisi) na ambavyo vipo ndani ya nchi na vimefanya usajili kufuatia kanuni ya idadi ya wachezaji.

2.2.2.4.3 ***Vilabu vya nje ya nchi***

Hivi ni vilabu toka nje ya nchi ambavyo usajili wa klabu na wachezaji huthibitishwa na mashirikisho wanakotoka, malipo yao hufanyika kwa kiwango cha kimataifa.

Masharti ya Muhimu

2.2.2.4.3.1 Kwasababu za kiufundi, klabu ya ndani ya nchi itafanya malipo ya ada ya ushiriki wa mashindano ya wazi kwa kiwango kilichopangwa kwa kundi la hapo juu (2.2.2.4.2) iwapo idadi ya wachezaji wakigeni itakuwa ni watatu (3).

2.2.2.4.3.2 Ikitokea Wachezaji wakigeni wanazidi watatu (3), malipo ya ada ya ushiriki yatabadirika na kufuata kiwango kilichopangwa kwa kundi la vilabu toka nje ya nchi (2.2.2.4.3),

2.2.3 **Ada za Usajili wa Muda - Temporary Transfer Fee**

Ada za usajili wa muda zitazingatia aina ya mashindano yaliyopo, jumla ya Tsh. 30,000/= zitalipwa kwenye akaunti ya TAVA. Mgawanyo utakuwa kama ifuatavyo;

2.2.3.1 Chama cha Mkoa kitalipwa asilimia arobaini (40%) Tshs. 12,000/=

2.2.3.2 Chama cha taifa – TAVA kitalipwa asilimia sitini (60%) Tshs. 18,000/=

2.2.3.3 Klabu anayotoka na anayokwenda watafanya makubaliano ya gharama za uhamisho wa mchezaji na kulipana wenyewe

2.2.3.4 Klabu inayomsajili mchezaji itafanya makubaliano ya gharama ya malipo kwa mchezaji husika katika uhamisho huo

2.2.3.5 Makubaliano yoyote kati ya hayo hapo juu lazima yafanyike kwa maandishi na kuwasilisha nakala za malipo na mktaba wa uhamisho kwenye chama cha mpira wa wavu taifa – TAVA kupitia chama cha Wilaya na Mkoa husika.

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

2.3 <u>Usajili wa Mchezaji kutoka nje ya nchi kwaajili ya ligi</u>

Klabu yoyote itaruhusiwa kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi kwaajili ya mashindano ya kitaifa na kimataifa, na mashindano ya wazi. Masharti ya usajili ya wachezaji hawa wakigeni yatakuwa kama ifuatavyo;

2.3.1 Klabu itafuata taratibu za nchi kuhusiana na uhamiaji wa raia wa kigeni,

2.3.2 Klabu haitaruhusiwa kusajili wachezaji wa kigeni zaidi ya watano (5) watakaotumika katika kikosi chake kitakachoshiriki ligi,

2.3.3 Taarifa za wachezaji wakigeni ziwasilishwe TAVA kwa maandishi kabla ya mchezaji kupewa leseni kuitumikia klabu yake, taarifa zitakazo wasilishwa ni pamoja na;

2.3.3.1 Paspoti ya mchezaji,

2.3.3.2 Taarifa ya timu anapotoka na anapokwenda mchezaji ikiwa ni ridhaa ya kuondoka/ makubaliano, ili kujaziwa ITC

2.3.3.3 Malipo ya mchezaji wa kigeni ni Tsh. 50,000/=

MUHIMU:

TAVA itatoa vitambulisho na leseni kwa waliokamilisha usajili. Timu, wachezaji, makocha na waamuzi. Waliosajiliwa ndiyo watakaoruhusiwa kushiriki mashindano yanayoandaliwa na kusimamiwa na TAVA kwa msimu husika.

2.4 <u>Utaratibu wa Malipo</u>

Malipo yote ya usajili na ada za uhamisho yafanyike kupitia akaunti ya **TAVA** iliyopo **NMB BANK** yenye taarifa zifuatazo;

a) Namba - **24510025069**
b) Jina - ***Tanzania Volleyball Association***

3. HAKI NA USIMAMIZI WA HADHI ZA WACHEZAJI

3.1 <u>Hadhi za Wachezaji na Makocha</u>

3.1.1 Mchezaji na Kocha atalindwa kupitia haki za asili za mkataba walioweka baina yao na Klabu. Upande mmoja wapo utakuwa na haki ya kufungua shauri kwaajili ya kupata haki kulingana na ukiukwaji wa mkataba baina yao.

3.1.2 Hatua za utafutaji haki baina ya pande mbili utafuata taratibu zifuatazo;

3.1.2.1 Klabu itakuwa ndiyo hatua ya awali kwaajili ya kusuluhisha migogoro,

3.1.2.2 Ikiwa suluhisho halijapatikana, mlalamikaji atapeleka malalamiko yake kwa kwa maandishi kwa Mwenyekiti wa Mkoa,

3.1.2.3 Ikiwa suluhisho halijapatikana, mlalamikaji atapeleka malalamiko yake kwa maandishi kwa Mwenyekiti - kamati ya Mashindano ya TAVA.

3.1.2.4 Ikiwa suluhisho halitafikiwa, mlalamikaji atapeleka malalamiko yake kwa maandishi kwa Mwenyekiti – Sekretarieti ya TAVA.

3.1.2.5 Ikiwa suluhisho halitafikiwa, mlalamikaji atapeleka malalamiko yake Baraza la Michezo la Taifa,

3.1.2.6 Ikiwa suluhisho halitapatikana katika hatua zote hizo, Katibu Mkuu wa TAVA atashauriana na Katibu Mkuu wa BMT kuruhusu mlalamikaji kutafuta haki yake kupitia mahakama. Aidha hukumu itakayotolewa na mahakama dhidi ya upande wowote wa shauri itapokelewa na kutekelezwa kwa mujibu wa kifungu cha 3.2

3.2 <u>Adhabu za ukiukaji wa mikataba au makubaliano</u>

3.2.1 Mdau yeyote aliyesajiliwa na TAVA kujihusisha na Mpira wa wavu atapaswa kufuata sheria za nchi zinazosimamia mikataba, na atapaswa kuheshimu makubaliano yaliyomo kwenye mkataba baina yao.

3.2.2 Mchezaji au kocha akivunja mkataba au makubaliano yaliyomo kwenye mkataba atawajibishwa kwa yote au moja wapo kati ya yafuatayo;

3.2.2.1 Kufungiwa usajili kwa msimu mzima ulioanza au unaotarajiwa kuanza.

3.2.2.2 Kulipa faini ya Tsh. 200,000/= ambayo atailipa TAVA.

3.2.2.3 Kulipa muathirika (Klabu) thamani ya athari kulingana na mahesabu yatakayowasilishwa na mlalamikaji. Aidha, thamani hiyo isizidi kiwango cha fedha ya usajili iliyolipwa au kupanga kulipwa kwaajili ya usajili wa awali).

3.2.3 Klabu itakayokiuka makubaliano ya mkataba baina yake na kocha au mchezaji itawajibika kwa adhabu moja au zote kama ifuatavyo;

3.2.3.1 Klabu itafungiwa kufanya usajili kwa msimu ulioanza au unaotarajiwa kuanza,

3.2.3.2 Klabu itatozwa faini ya Tsh. 500,000/= ambayo atailipa TAVA.

3.2.3.3 Klabu itamlipa muathirika thamani ya athari kulingana na mahesabu yatakayowasilishwa na mlalamikaji. Aidha, thamani hiyo isizidi kiwango cha fedha ya usajili iliyolipwa au kupanga kulipwa kwaajili ya usajili wake).

3.2.4 Klabu, Mchezaji au Kocha ataondolewa adhabu endapo atashinda kufuatia rufaa atakayoiweka, na adhabu zote zitafutwa.

3.2.5 Ikiwa malalamiko yanahusiana na malipo kwa pande mojawapo, adhabu ya kufungiwa usajili na ya kumlipa faini muathirika zitakayoondolewa. Adhabu ya faini kwa TAVA (3.2.2.2 na 3.2.3.2) itapaswa kutekelezwa, na ikiwa adhabu hii haitatekelezwa,

mlalamikiwa ataendelea kutumikia adhabu ya kufungiwa (3.2.2.1 na 3.2.3.1) kama inavyojieleza.

4. HITIMISHO

Nimatumaini ya chama cha mpira wa wavu Tanzania kuwa wadau wote watashiriki katika kuhakikisha kanuni hizi zinatekelezwa, na Kwasababu ya uboreshaji endelevu (continuous improvement), TAVA haitafunga milango yake kupokea maoni na ushauri kwaajili ya kuboresha kanuni zake ili kufanya mchezo wa mpira wa wavu kuvutia wadau wote. Kwa changamoto zozote toka kwa mdau wasilisha kupitia Kamisheni ya ufundi au anuani zilizopo kwenye waraka huu.


Laurence Safari
Katibu Mkuu

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 DAR ES SALAAM

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578

- Anuani ya Usajili ya TAVA - https://register.tvf.or.tz/

NAMNA YA KUINGIA KUJISAJILI KUTUMIA KOMPYUTA




HATUA YA 1 NI KWA MENEJA WA KLABU KUFUNGUA AKAUNTI KWA KUBONYEZA ALAMA HII.

MENJA AKISHABONYEZA HAPO UTAFUNGUKA UKURASA AMBAO ATAPASWA KUINGIZA TAARIFA ZAKE ZITAKAZO MRUHUSU KWENDA HATUA NYINGINE

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578



2

JAZA TAARIFA ZAKO KWA UFASAHA KATIKA KILA NAFASI ILIYOWAZI. SOMA MAELEKEZO CHINI KILA BOX

WEKA BARUA INAYOKUTAMBULISHA KUWA WEWE NDIYO MENEJA WA KLABU. USIPO AMBATANISHA BARUA HIYO TAARIFA HIZI HAZITATOKA KWENYE UKURASA WAKO


3

4

HATUA YA 4 UKIWA UMEJAZA TAARIFA ZOTE KWA UFASAHA NA KUAMBATANISHA BARUA YA UTAMBULISHO UTABONYEZA KITUFE HIKI. ANGALIZO, KAMA KUNA KIPENGELE HUJAJAZA UKURASA HUU UTAGOMA KUTUMWA NA ITAKULETEA UJUMBE


TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578



HATUA YA 5 – TAARIFA YAKO IKITUMWA KWA UFASAHA, UTAPEWA UJUMBE HUU HAPOHAPO.

UTAPOKEA UJUMBE KUPITIA EMAIL ULIYOISAJILI WAKATI UNAJAZA TAARIFA HATUA YA 2 HAPO JUU




HATUA YA 6 – FUNGUA EMAIL YAKO UTAKUTA UJUMBE KUTOKA TAVA

UTAPASWA KUBONYEZA HIYO LINKI AMBAYO ITAKUPELEKA KWENYE UKURASA MPYA UTAKAOKUPATIA NAFASI YA KUINGIZA USER NAME MPYA NA KUKUPA PASWORD YA KUINGILIA

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578




HATUA YA 7 – UTARUDI KWENYE UKURASA WA KWANZA NA UTAINGIZA USER NAME NA PASSWORD ULIZOJAZA KWENYE HATUA YA SITA HAPO JUU. UKIINGIZA UNABONYEZA LOG IN.

HAKIKISHA UNATUNZA PASSWORD ZAKO NA USER NAME

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578




HATUA YA 8 – CHAGUA NENO TEAMS, CHINI YAKE KUNA KITUFE KIMEANDIKWA ADD NEW, BONYEZA.

HAPO ZITAFUNGUKA KURASA UPANDE WA KULIA KWAJILI YA KUJAZA TAARIFA ZA TIMU YAKO

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578

8



TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578

FOMU YA MAKUBALIANO KATI YA MCHEZAJI NA TIMU

BAINA YA

JINA LA TIMU……..…… ANUANI……

NA

JINA LA MCHEZAJI……...……...…… ANUANI……

Kwakuwa timu husika inashiriki michuano mbalimbali inayosimamiwa na Chama cha Mpira wa Wavu Tanzania (TAVA), kwa kuwa timu husika inayo nia ya kumsajili mchezaji husika kwa kipindi cha msimu wa……, Kwa kuwa mchezaji ameafiki kusajiliwa na timu husika, na kwa kuwa MCHEZAJI na TIMU wote wameishajadiliana na kukubaliana na usajili huo.

MASHARTI YA MAKUBALIANO

1. Tarehe ya kuanza mkataba……/……/…….. Hadi terehe……/……/……
2. Thamani ya mkataba…… (Ikijumuisha Ada ya usajili na malipo mengine kama yapo)
3. Uthibitisho wa malipo husika kama yamefanyika. Ndio …….. Hapana……...
4. Mshahara kwa mwezi…… Utakaolipwa kila tarehe…… (Iandikwe mtumishi wa taasisi iwapo hakuna mshahara maalumu ya kiuchezaj)
5. Mchezaji kutosajiliwa na timu nyingine bila makubaliano ya pande zote mbili isipokuwa akipata ajira katika taasisi iliyo na timu na kutakiwa kutumikia taasisi hiyo
6. Mchezaji atakubaliwa kuwa mchezaji halali wa klabu hadi itakapo ridhiwa na TAVA.

WAJIBU WA TIMU KWA MCHEZAJI

1. Kumsajili katika mfumo wa TAVA kuwa mchezaji halali ikijumuisha malipo yote stahiki kwa TAVA na kwa mchezaji mwenyewe, pamoja na kuwasilisha nyaraka zote muhimu TAVA ikiwa ni pamoja na kuhakikisha anapata namba ya usajili wa wachezaji kutoka TAVA
2. Kumpatia mahitaji yote muhimu, hasa jezi za timu na vifaa vingine vya michezo kwa namna watakavyokubaliana.

WAJIBU WA MCHEZAJI KWA TIMU

1. Kucheza na kujituma, kuwa na juhudi na maaarifa, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria programu za mazoezi za timu kwa mujibu wa maagizo ya timu.
2. Kuwa na nidhamu ya juu wakati wote wa utumishi wake kama mchezaji, ikiwa ni pamoja na kutunza vema mali za timu.
3. Kuwa msiri juu ya makubaliano baina yake na timu.

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION P. O. Box 10496 Dar Es Salaam, Tanzania.
Tel: +255 784 828 645 / +255 685 267 578

SABABU ZA USITISHWAJI WA MAKUBALIANO KWA HARAKA

1. Endapo utatokea ukiukwaji wa kama ilivyo ainishwa katika makubaliano haya hapo juu.
4. Upande mmoja kuamua kusitisha makubalino na kulipa gharama stahiki (Mchezaji kwa Timu) au kiasi cha fedha kilichosalia katika mkataba kuisha (Timu kwa Mchezaji) ikijumuisha pia mshahara wa miezi iliyobaki katika mkataba wake au malipo mengine katika makubaliano yao mengine.

Imesainiwa kwa niaba ya **TIMU**

Eneo: ……

Tarehe Mhuri wa Timu

NA

Jina: ……

Sahihi: ……

Anuani ya Posta: ……

Cheo: ……

SHUHUDA

Jina: ……

Sahihi: ……

Anuani ya Posta: ……

Imesainiwa na **MCHEZAJI**

Eneo: ……

Tarehe ……
SAHIHI YA MCHEZAJI

SHUHUDA

Jina: ……

Sahihi: ……

Anuani ya Posta: ……

TANZANIA VOLLEYBALL ASSOCIATION